

KUISHI, KUFA, KUZIKWA, KUFUFUKA, KUJA

 Ni zaidi ya kitu cho chote tungaliweza kueleza katika lugha za binadamu jinsi mioyo yetu inavyosikia leo tunapokusanyika hapa asubuhi hii tukufu na iliyo ya kiungu sana. Asubuhi hii inawakilisha wakati ambapo dini yetu ilifanywa ya kweli, kwa maana ilikuwa kufufuka tena kwa Mwanao Mpendwa Ambaye alikuja kukomboa jamaa yote ya binadamu. Nasi tuko hapa asubuhi ya leo katika kusherehekea wakati huo ulio mkuu sana, Bwana, uliotufanya kuwa zaidi ya washidi wa mauti, kuzimu na kaburi. Nasi tunakushukuru kwa kuwa, hata baada ya miaka hii yote kupita, tungali tunakusanyika mapema katika asubuhi hii ya Pasaka, kumwabudu Yeye, kwa sababu tunaamini ya kwamba Yeye atakuja tena.

² Nasi tungeomba ya kwamba ungetusamehe dhambi zetu zote na makosa yetu yaliyorekodiwa dhidi yetu, tunapoungama kwa unyenyekevu makosa yetu, na kukubali upatanisho Wake kwa dhambi zetu. Waponye wagonjwa walio miongoni mwetu, Bwana. Tusaidie tunaposoma Neno Lako Takatifu, ambalo ni msingi wa Kweli zote ambazo umetuachia kuishi kwazo na kuamini.

³ Nasi tunaomba si kwa kundi hili tu lililokusanyika hapa, bali kote ulimwenguni, kwa maana tunatazama kwa macho yenye hamu na mioyo yenye matumaini kule kurudi Kwake. Tunasimama siku hizi katika giza, na machafuko, ambapo, wakati wo wote, mwenda wazimu anaweza kukasirikia jambo fulani, na kufinya mtambo mdogo, na ulimwengu mzima ungelipuliwa vipande vipande. Kama vile tumekwisha kuambiwa na wataalam wakuu, ya kwamba, vita vitachukua tu masaa machache, kama vitatukia tena. Lo! Nasi tuko ukingoni mwa vita vingine. Kisha, kanisa linasimama ukingoni, ule ufufuo wenye utukufu sana, kwa kuwa tutanyakuliwa pamoja na watakatifu waliolala, kumlaki Bwana hewani, kisha tuwe pamoja naye milele.

⁴ Tumekuja kukuabudu, Bwana. Na utupokee leo. Bariiki kusomwa kwa Neno, kuimbwa kwa nyimbo, kuhubiriwa kwa Injili, pokea maombi ya wenye toba. Yasikie maombi ya walio wagonjwa, na ukipatie utukufu, kwa sababu tunaomba kwa unyenyekevu katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

⁵ Kwenu ninyi ambao mngetaka kuchukua mahali ambapo tungenesoma asubuhi hii, kwa Maandiko yetu.

⁶ Nasi tunasikitika ya kwa—kwamba tunajua hatuna nafasi ya kuketi kwa ajili ya hili kundi nzuri la watu ambao wamekuja mapema asubuhi hii kuabudu pamoja nasi, kutoka makanisa mbalimbali na kutoka mikoa mbalimbali, na hata mataifa mbalimbali, wamekusanyika asubuhi ya leo hapa kwenye Maskani kwa ajili ya hii ibada tukufu sana ya Bwana.

⁷ Nataka kufungua Kitabu cha Zaburi, Zaburi 22. Najua hapa ni mahali pasipo pa kawaida kusoma, kwa ajili ya ibada ya Pasaka, bali Mungu si wa kawaida.

⁸ Na sasa baada ya ibada hii, tutaahirisha kwa yapata saa moja, kusudi mpate kwenda kula kiamsha kinywa chenu. Ndiposa ibada ya shule ya Jumapili itaanza saa tatu u nusu. Kisha mara baada ya shule ya Jumapili, kutakuweko na ibada ya ubatizo hapa kwe—kwenye kidimbwi. Kisha leo alasiri, saa kumi na mbili, kadi za maombi zitatolewa kwa ajili ya ibada ya uponyaji usiku wa leo. Na iwapo una ye yote unayempenda ambaye ni mgonjwa na mhitaji, kumbukeni kuwaleta usiku wa leo, kwa sababu huu utakuwa ndio wakati wa mwisho tutakaokuwa nayo kwa—kwa muda fulani, kwa vyo vyote. Ninaondoka kesho asubuhi, saa kumi na moja, kuelekea Los Angeles na kuzuru Pwani ya Magharibi, kwa mfululizo wa ibada.

⁹ Basi katika Zaburi 22, tutasoma,

Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?

Mboma U mbali na wokovu wangu, . . . na maneno ya kuugua kwangu?

Ee Mungu wangu, nalia mchana lakini hujibu; Na wakati wa usiku lakini sipati raha.

Na Wewe U Mtakatifu, Uketiye juu ya sifa za Israeli.

Baba zetu walikutumaini Wewe, Walikutumaini, na Wewe ukawaokoa.

Walikulilia Wewe wakaokoka, Walikutumaini wasiaibike. Lakini mimi ni mdudu wala si mtu. Laumu ya wanadamu . . . mzaha wa watu.

Wote wanionao hunicheka sana, Hunifyonya, wakitikisa vichwa vyao;

Husema, Umtegemee Bwana; na amponye, Na amwokoe sasa, maana apendezwa naye.

Naam, Wewe ndiwe uliyenitoa tumboni, Ulinitumainisha matitini mwa mama yangu.

Kwako nalitupwa tangu tumboni, Toka tumboni mwa mamangu ndiwe Mungu wangu.

Usiwe mbali nami maana taabu i karibu, Kwa maana hakuna msaidizi.

Mafahali wengi wamenizunguka, Walio hadari wa Bashani wamenisonga; Wananifumbulia vinywa vyao, Kama simba apapuraye. . . na kunguruma.

Ninamwagika kama maji, . . . Mifupa yangu yote imeteguka, Moyo wangu umekuwa kama nta, Na kuyeyuka ndani ya mtima wangu.

Nguvu zangu zimekauka kama gae, . . . Ulimi wangu waambatana na taya zangu; Unaniweka katika mavumbi ya mauti.

Kwa maana mbwa wanenizunguka, Kusanyiko la waovu wanenisonga; Wamenizua mikonono na miguu.

Naweza kuihesabu mifupa yangu yote; Wao wanitazama na kunikodolea macho.

Wanagawanya nguo zangu, . . . Na vazi langu wanalipigia kura. Nawe Bwana, usiwe mbali, Ee nguvu zangu, fanya haraka kunisaidia.

Uniponye nafsi yangu na upanga, Mpenzi wangu na nguvu za mbwa.

Kinywani mwa simba uniokoe, Naam, toka pembe za nyati umenijibu.

Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu, Katikati ya kusanyiko nitakusifu.

Ninyi mnaoamcha BWANA, msifuni, Enyi nyote mlio wazao wa Yakobo, mtukuzeni, Mcheni, enyi nyote mlio wazao wa Israeli.

Maana hakulidharau teso la mteswa, . . . Wala hakuchukizwa nalo; Wala hakumficha uso wake, Bali alipomlilia akamsikia.

Kwako zinatoka sifa zangu Katika kusanyiko kubwa. Nitaziondoa nadhiri zangu Mbele yao wamchao.

Wapole watakula na kushiba, wamtafutao BWANA watamsifu; mioyo yenu na iishi milele.

Miisho yote ya dunia itakumbuka, Na watu watamrejea BWANA; Jamaa zote za mataifa watamsujudia.

Maana ufalme una BWANA, Naye ndiye awatawalaye mataifa. Wakwasi wote wa dunia watakula na kusujudu, Humwinamia wote washukao mavumbini; Naam, yeye asiyeweza kujihuisha nafsi yake,

Wazao wake watamtumikia. Zitasimuliwa habari za BWANA, kwa kizazi kitakachokuja,

Watakuja nao watawahubiri na wata- . . . watakaozaliwa haki yake, ya kwamba ndiye aliyeyafanya.

¹⁰ Bwana na aongeze baraka Zake kwa kusomwa kwa Neno Lake. Nataka kuchukua wakati huu asubuhi ya leo, maneno matano, na kwa maneno hayo nijaribu kueleza yaliyo moyoni mwangu, kwa ninyi waabuduo asubuhi ya leo. Nayataka haya maneno matano: *Kuishi, Kufa, Kuzikwa, Kufufuka, Kuja*.

¹¹ “Nafikiri yule mshairi aliyaeleza vyema katika wimbo, yale ningetaka kusema, alipouandika huu wimbo.

Maishani, alinipenda. Kufani, akaniokoa.
Alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu.
Alipofufuka, akanihesabia haki bure milele.
Yuaa siku moja, lo, siku tukufu!

¹² Hamna maisha yaliyoishiwa kama Yake, kwa sababu alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili alipozaliwa. Yeye alikuwa onyesho la kile alichu Mungu Baba. Na Mungu Baba akiwa upendo, basi Yesu alikuwa maonyesho yote ya upendo. Yeye alikuwa upendo tangu mara ya kwanza ambapo mikono yake midogo ya kitoto ilipozipapasa zile shavu nzuri za mamaye. Yeye alikuwa upendo.

¹³ Nami nafikiri leo ya kwamba hapo ndipo wengi wanakosea kutambua ya kwamba Yeye alikuwa upendo. “Mungu ni upendo, na hao wapendao wamezaliwa na Mungu.”

¹⁴ “Mungu aliupenda ulimwengu, hiyo ni kusema, usiopendeka, hata akamtoa Mwanaye pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele.”

¹⁵ Yeye alionyesha upendo Wake alipokuwa hapa duniani, katika njia nyingi tofauti, hata haiwezi kubishaniwa ya kwamba Yeye alikuwa kiumbe mwenye upendo sana aliyepata kuishi. Nami nafikiri, katika maisha Yake hapa, Yeye alikuwa akimwonyesha Mungu. Na njia pekee Mungu anayoweza kuonyeshwa kwa watu ni kwa upendo.

¹⁶ Naye alifanya hili vizuri alipomshika labda mmoja wa wanawake waovu sana waliokuweco katika siku Zake. Wao walimpata na hatia, na hapakuwepo njia ya kuepukia, aliposhikwa katika uzinzi. Nao wakamkokota mbele Zake, na kusema, “Wasema tumfanyie nini?”

¹⁷ Na Yeye alipomgeukia, akasema, “Sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena.” Badala ya kumtupa nje barabarani akakokotwe kama kundi la mbwa mwitu juu yake, kumpiga mawe na kutoa uhai wake; moyo Wake mpole, wenye huruma na upendo ulinama chini katika hiyo dhambi aliyokuwemo, kasema, “Mimi sikuhukumu. Nenda zako tu na usitende dhambi tena.”

¹⁸ Na alipokuwa akishuka kwenda kaburini mwa Lazaro, nafikiri huo ulikuwa wakati mwingine mkuu alipoonyesha jinsi Mungu alivyo kwa wanadamu. Yeye si Mungu tu anayoweza kusamehe dhambi iliyo baya sana inayoweza kutendwa, na

kuchukua hatia na kuwafanya wasio na hatia, kwa upendo Wake unaosomehe. Bali baada ya mauti kutunyamazisha, Yeye yu angali anatushughulikia. Nafikiri alionyesha hayo vizuri alipokuwa njiani pamoja na Maritha na Mariamu, alipofika kwenye nyumba ambamo mauti yaliisha kukomesha uhai wa mtu mpendwa. Na alipokuwa njiani kuelekea kaburini, ingawaje, akiwa Mungu, alijua ya kwamba angemfufua kutoka kwa wafu, alijua ya kwamba alikwisha kuambiwa ya kwamba katika Neno Lake mlikuwemo Uweza kumfufua toka kaburini, hata hivyo, alipowaona Maritha na Mariamu na wale waliompenda Lazaro, wakilia, Biblia ilisema Yeye alilia. Ilikuwa nini? Moyo Wake mkuu wenye upendo! Alipoona ya kwamba watu na rafiki za—zake walikuwa wanahangaika Yeye akahangaika pamoja nao.

¹⁹ Nina furaha sana kujua ya kwamba Yeye anaweza kupatikana miongoni mwa waliovinjika mioyo. Na katika huzuni zetu, Yeye si anayeweza kutuacha. Yeye husimama pamoja nasi wakati yote yameshindwa, na matumaini ya mwisho ya kidunia yafikiapo mwisho, Yeye yu angali Mungu na hutupenda. Yeye alikuwa wonyesho wa Mungu.

²⁰ Na, lo jinsi ninavyoamini ya kwamba Yeye ana shauku kwa watu Wake kuwa na upako sana wa Roho Mtakatifu, hata tungeweza kuendana sisi kwa sisi katika majaribu na shida, na kuonyesha huruma Zake, zikitoka mioyoni mwetu iliyozaliwa na Roho Wake, kuonyesha kanisani upendo wa Mungu aishiye. Hayo yameelezwa vizuri na yale Yeye aliyosema, ama yule mshairi alivyosema.

Maishani, alinipenda.

²¹ Naye akaonyesha yale aliyowatendea binadamu wote, jinsi Mungu alivyojiwakilisha katika Yesu Kristo. Yeye alitoa maoni Yake kwa jamii ya binadamu, kusamehe na kuwapenda wale wasiopendeka. Nami nashangaa, katika asubuhi hii ya Pasaka, jinsi tumepungukiwa na hayo. Tungewapenda hao watupendao, bali Yeye aliwapenda hao wasiopenda.

²² Yeye alikuwa ndiye mkuu sana, uwakilisho wa kwanza, wa upendo uliowahi kuja ulimwenguni; naye alidhihakiwa na wale walioishi duniani, ambao aliwapenda. Hamna mtu angaliweza kupenda kama Yeye; na hamna mtu aliyepata kuchukiwa kama Yeye. Wao walimchukia na kumdhihaki, na kumkataa, bali haikukomesha upendo Wake. Walimchekelea, alipokuwa amening'inia msalabani, baada ya maisha hayo aliyokuwa ameishi kutotenda neno ila mambo mazuri, akisamehe wenye hatia, akiwaponya wagonjwa, na mambo tu yaliyokuwa mema. Alipokuwa...kupumua kwa mwisho msalabani, pamoja na kuzungukwazungukwa, mate aliyotemewa ya kumdhihaki, ya wale waliosimama karibu; akining'inia, na kutoka kwa uso

Wake mtakatifu Yeye alilia, na moyo uliojaa upendo, “Baba, wasamehe, kwa kuwa hawajui watendayo.”

²³ Yeye angefahamu. Akiwa Mungu, Yeye anafahamu. Hiyo ndiyo sababu Yeye anatupenda tukiwa tusiopendeka, kwa sababu Yeye ni Mungu naye anafahamu. “Maishani, alinipenda.” Hamna maisha yaliyoishiwa kama hayo, kwa sababu yalikuwa yamefunikwa katika upendo.

Kifoni, akaniokoa.

²⁴ Mauti, walipokuwa katika Bustani ya Edeni, Mungu Aliye Yehova aliyahitaji. Adhabu ya dhambi ni mauti, na hukungekuweko ubadilisho. Haingalishungulikiwa kwa njia nyingine yo yote. Kwa maana, Mungu ni mkuu, naye hana kikomo, na Hakimu wa Mbingu zote na nchi. Adhabu ya dhambi ni mauti, na hamna mtu angaliweza kulipia mwingine adhabu hii. Kwa maana kila mtu, ingawa huenda akafa kwa ajili ya mtu mwingine, bali kwanza alikuwa mwenye hatia. Hapakuwepo mmoja wetu ambaye angemsaidia mwingine, kwa maana sote tulikuwa wenye hatia. “Tulizaliwa dhambini, tukaumbwa katika uovu, tukaja ulimwenguni tukinena uongo.” Na hapakuwepo tumaini hata kidogo, po pote. Tulikuwa tumehukumiwa kifo, na Mungu, na kila kiumbe kilichopata kutembea duniani kilikuwa chini ya hukumu hii. Watu wenye haki wangeinuka na kufanya mambo makuu, bali kwanza ni mwenye dhambi.

²⁵ Kulikuweko njia moja tu ya kuilipia, na hiyo ilikuwa mauti ya Mungu Mwenyewe. Kwa hivyo Mungu, akiwa Roho, hangalikufa, bali alishuka katika mwili wa nyama na kujionyesha Mwenyewe katika maisha ya upendo; kutwaa wema huo wote ambao alikuwa, na kuutoa kwa hiari Yake kama dhabihu iliyo kuu sana, apate kuchukua hatia ya wenye hatia. Sote tulikuwa wenye dhambi, na hapakuwepo njia ulimwenguni kwetu kuokolewa kamwe. Yeye alikuja si kuonekana tu duniani, bali alikuja apate kufa kama Dhabihu.

²⁶ Habili alionyesha hilo alipomtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; alipomleta maskini mwana-kondoo yule mwambani, huku amefungwa shingoni kwa kipande cha mzabibu. Hapo alilala yule mnyama masikini juu ya mwamba, akavuta nyuma kidevu chake kidogo na, kwa—kwa jiwe, akatwanga koo lake ndogo; huku akilia na kufa, damu ikimdondoka, kipande hiki kidogo cha jiwe kikalowa damu. Habili alionyesha kalvari hapo.

²⁷ Wakati Mwana-kondoo wa Mungu, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, alipokuja kupachukua mahali pa wenye dhambi walio na hatia, naye akapondwa-pondwa na kujeruhiwa, na—na kuchekelewa na kudhihakiwa, na kufa kifo ambacho hamna kiumbe kingeliweza kufa ila Mungu Mwenyewe, na nywele zake zilizolowa damu zikining’inia

mabegani Mwake, ikitiririka ardhini, ilionyesha jinsi dhambi ilivyo jambo la kuogofya, ilipombidi kufa apate kumkomboa mwanadamu kutoka kwa maisha ya dhambi. Hakuna kitu kingeliweza kufa hivyo. Hakuna kitu kingelistahimili hayo mauti. Inasemwa kuwa, “Walipomchoma umbavuni, kulitoka Damu na Maji.”

²⁸ Hivi majuzi, nilikuwa nikimzungumzia mtu fulani juu haya. Na ilikuwa mwanasayansi aliyesema, “Mna njia moja ambayo hayo yangalitendeka. Na haikuwa kwa sababu ya mkuki wa Kirumi, ili afe; wala haikuwa kwa kupoteza Damu, ili afe, kwa maana kulikuwa kungali Damu mwilini Mwake. Kilichomuua, haikuwa kwa sababu ya mkuki wa Kirumi ama misumari aliyopigiliwa mikononi Mwake, ama taji ya miiba waliyoiweka kichwani Mwake. Bali kwa sababu . . . Yeye aliuwawa na huzuni, kwa maana alikuja Kwake, wala walio Wake hawakumpokea. Alikufa kwa kuvunjika moyo. Wakati, Yeye alijua ya kwamba wale viumbe wa wakati, ambao angekufa apate kuwakomboa, waliisha mtemea mate usoni Mwake, naye alikataliwa na wanadamu.”

²⁹ Daudi, miaka mia nane kabla haijatendeka, alilia kwa sauti ile ile Yeye aliyolia kwayo kule Kalvari, “Mungu Wangu, mbona umeniacha?”

³⁰ Ni jambo baya jinsi gani dhambi ifanyalo, inatenganisha mwanadamu na Mungu! Naye alikuwa toleo la dhambi lililopaswa kutolewa kwa ajili ya dhambi zetu. Naye alitengwa na Uwepo wa Mungu. Dhambi ilimtenganisha Yeye. Mungu aliweka dhambi zetu juu Yake, naye akatenganishwa na Mungu, na hiyo ndiyo sababu Yeye alilia, “Mbona umeniacha?” Na kwa sababu alikuwa amekwisha achwa, na alikuwa amechukua mahali hapa; na kuona watu Wake, ambao alikuwa amekuwa kuwa Mwokozi wao na kuwapa Uzima, wao walikuwa wamemkataa. Nayo ilimtia huzuni sana, hivi kwamba Yeye alivunjika moyo sana hata Damu na maji, na madawa ya mwili Wake, vilitengana.

³¹ Binadamu hatajua kamwe hiyo ilikuwa nini. Hiyo ndiyo sababu hamna mtu mwingine ye yote angalikufa hivyo. Sijali ungaliteswa vipi, jinsi wangelitia miguu yako kwenye mkatale, au kukukata kwa msumeno inchi kwa inchi, au kukuchomwa moto inchi kwa inchi; haungalikufa kifo hicho, kwa sababu muundo wako hauko hivyo. Iлимпasa kuwa Mungu. Iлимпasa kuwa zaidi ya mwadamu; katika njia, Mungu aliyokufa. Yeye alikufa kwa kuvunjika moyo, huzuni nyingi sana juu ya ulimwengu, hata vituko vyo madawa vikatukia Mwilini Mwake ambavyo havingalitukia kwako. Wewe huwezi kuteseka hivyo. Hamna njia kwako kupata huzuni ya aina hiyo. Kwa hivyo kuna Mmoja tu angaliweza kufanya hivyo, na alifanya.

³² Ndio huo ukininginia pale, ule uzima wa dhamani ambao haukujua cho chote bali upendo na kutenda mema, ukining'inia pale kati ya Mbingu na nchi, aliinuliwa, juu pale, alivuliwa nguo, alitahayarishwa. Wazia jinsi ungekuwa, huku umevuliwa nguo; haungalitahayarika jinsi Mungu alivyotahayarika, aking'inia pale. Najua ile sanamu ya kuangikwa msalabani ina kitu kidogo, wao wamemzungushia kitu fulani, bali hawakufanya hivyo kamwe, hicho kimewekwa mle kwa sababu mchoraji alikiweka mle. Walimvua nguo Zake. Alikuwa amevalia joho, nao wakamvua hilo na kulipigia kura. Yeye alitahayarishwa, vilivyo. Hata hivyo, akiwa Mungu, ilimpasa kusimama na wenye dhambi kumtemea mate usoni Mwake. Hata hivyo akiwa—akiwa kilindi cha rehema, ilimpasa kufa mbele ya umma, uchi wa mnyama. Matokeo yake yalikuwa mabaya sana Kwake hata yakatenganisha maji na Damu. Si ajabu...nafikiri mshairi aliyaonyesha hayo vizuri aliposema:

Huku miamba ikipasuka, na mbingu zikiwa
giza, Mwokozi wangu aliinamisha kichwa
Chake akafa,

Bali pazia lililofunguka ilifunua njia ya
kuingia kwenye raha za Mbinguni na siku
isiyo na mwisho.

³³ Bila shaka, ilimpasa kufanya hivyo. Hiyo pazia ilining'inia kati ya wanadamu na Mungu, na hiyo pazia iliyofunguliwa ilifunua njia ya raha za Mbinguni na siku isiyo na mwisho. Kalvari inamaanisha kitu fulani, inamaanisha zaidi ya yale tungaliweza kutamka. Bila shaka.

Maishani, alinipenda. Kifoni, akaniokoa.
Alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu.

³⁴ Imehukumiwa sasa. Dhambi haina nguvu tena. Alipolia msalabani kwa sauti kuu, "imekwisha," dhambi ikafa! Sasa imekufa. Imemalizwa. Haina nguvu. Haina uhai. Wazieni hayo, enyi watu. Hiyo dhambi, adui wa binadamu, imekufa na haina uhai, haina nguvu tena. Haiwezi kuwa nazo. Jua lilipokoma kuangaza, nyota hazingalitoa nuru, nchi ikawa nyeusi, yote ilikuwa ikikombolewa.

³⁵ Sasa imekufa, imezikwa, haina uhai. Haina uhai ndani yake tena, basi haina budi kuzikwa. Ni nini kulichozikwa? Mwili wa Mungu ulizikwa, kwa maana Ulikuwa toleo la dhambi. Ulikuwa Mwana kondoo aliyeteketezwa, uliteketezwa na mioto ya uovu. Huyu Mwana-kondoo asiyejua dhambi yo yote, yule Mungu asiyejua makosa yo yote; uhai Wake ulikuwa umetolewa, kisha hapo likaning'inia toleo la dhambi, alipozikwa akaondolea mbali dhambi zangu. Ni lazima Azikwe. Ule mwili, lile toleo la dhambi halina budi kuzikwa.

³⁶ Hiyo ndiyo sababu wengi, baada ya kitambo kidogo, watakuja, mmoja kwa mmoja, kwenye kidimbwi hiki, kubatizwa

kwa Jina la Yesu Kristo. Kwa nini? Jambo fulani limetendeka. Huyu Roho aliyetoka kwenye mwili huo, wakati alipolia kwa sauti kuu “imekwisha,” ameihukumu dhambi miilini mwetu. Nasi hatuna budi kuizika, isikakumbukwe tena. Nina furaha sana kwamba ndivyo ilivyo.

³⁷ Wakati cho chote kimezikwa, kimefichwa, hakionekani. “Na alipozikwa, aliondolea mbali dhambi zangu.” Mungu hawezi tena kuona dhambi zetu, kwa maana zimezikwa. Zimezikwa wapi? Katika Bahari ya Usahaulifu. Waza kuhusu Bahari ya Usahaulifu! Mungu hawezi kuzikumbuka tena, kwa sababu zimekufa na kuzikwa pia. Haziwezi kukumbukwa tena. Mungu amezisahau.

³⁸ Pia Yeye alikuwa, katika huku “kuzikwa,” aliwakilisha Agano la Kale. Wao walikuwa na mbili... Walikuwa na toleo la dhambi katika kutakaswa kwa madhabahu. Na hilo toleo la dhambi lilikuwa kwamba wao walichukua mbuzi wawili, na mbuzi mmoja aliuawa; na huyo mbuzi mwingine, ile dhambi iliyowekwa juu ya yule mbuzi aliyekufa iliwekwa juu ya mbuzi aliye hai.

³⁹ Kumbuka, Yesu alikuwa Kondoo. Alikuwa Mwana-Kondoo, bali katika hali hii Yeye akawa mbuzi, alikuwa mwenye haki kwa sababu alikuwa Mungu, yule Kondoo. Bali akawa mbuzi, dhambi, apate kuwa toleo la dhambi kwa ajili yangu na yako; kutoka Kondoo hadi mbuzi.

⁴⁰ Naye Yesu aliwakilishwa katika wanyama wote wawili, mbuzi wote wawili. Kwa maana, mmoja, alikufa, alikufa kwa ajili ya upatanisho; wa pili, zile dhambi kutoka kwa upatanisho ziliwekwa juu ya mbuzi wa Azazeli, naye Azazeli akachukua dhambi za watu na akaenda mbali jangwani, kuchukua dhambi za watu. Ilikuwa nini? Ilikuwa kifo na kuzikwa kwa Bwana wetu Yesu. Kifoni! “Maishani, alinipenda. Kifoni, akaniokoa. Alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu.” Yeye alizichukua dhambi za watu, na kuzipeleka hadi kuzimu iliyo chini sana. Yeye alikuwa toleo la dhambi. Alikuwa na dhambi za watu. Alikufa kwa ajili yao. Pia dhambi iliwekwa juu yake, naye akaziondolea mbali dhambi zetu, mbali sana hata Mungu hangaliziona tena. Wazia hilo! Lo, Kanisa lingeweza kupaza sauti, “Haleluya kwa Mwokozi kama huyo!”

⁴¹ Dhambi zetu hazijasamehewa tu, bali zimezikwa katika Bahari ya Usahaulifu, zisikumbukwe tena. “Alipozikwa, akaziondolea mbali dhambi zetu.” Haziwezi kukumbukwa tena, kwa maana zimeondolewa. Zimeondolewa machoni pa Mungu. Zimepoozwa. Zimetaliwa. Zimetupwa mbali. Mungu hazikumbuki tena. Nini? Kanisa linapaswa kufurahi asubuhi ya leo, kujua ya kwamba dhambi zetu hazitakumbukwa tena. Zimewekwa katika bahari ya Usahaulifu, ndani ya kaburi ambamo haziwezi kufufuliwa tena. Zimekufa milele,

na kusahauliwa. Ni kama kwamba hazikutendeka kamwe. “Kifoni, akaniokoa. Lakini, alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu.” Alizichukua mbali sana hata zikaingia katika Bahari ya Usahaulifu. Lo! Tunajua ya kwamba mambo haya yanaaminiwa bila shaka kati yetu, na bila shaka ni Kweli. Ni Kweli ya Mungu. Hayo mambo yote makuu yangekuwa zaidi ya kuelezwa na mwanadamu. Hatungeweza kamwe kueleza shukrani zetu kwa mambo kama hayo.

⁴² Bali lo hiyo Pasaka! “Alipofufuka akanihesabia haki bure milele.”

Maishani, alinipenda. Kifoni, akaniokoa.
Alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu.
(Hiyo ilikuwa sawa).
Lakini, alipofufuka, akanihesabia haki.

⁴³ Huko kufufuka kulikuwa nini? Kulikuwa risiti ya Mungu, ya kwamba deni imelipwa. “Alipofufuka akanihesabia haki bure milele.” Lo, ni Mwokozi jinsi gani, aliyefufuka! Mungu alikuwa amefanyaje? Mtu anaweza kuteseka, mtu anaweza akafa, mtu anaweza akazikwa. Bali Pasaka ndiyo iliyokuwa kubwa zaidi ya zote, kwa maana ilikuwa kibali cha Mungu, “Sheria Zangu zimetimizwa, masharti Yangu yametimizwa Naye,” Yeye alimfufua kutoka kwa wafu! “Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele.” Jina lake Takatifu libarikiwe.

⁴⁴ Si ajabu inasababisha mwamsho! Si ajabu moyo wa mwanadamu hauwezi kuitoshea! Lo, kwa imani yetu ya ushindi tunaweza kusimama kule ng’ambo na kusema, “Sisi tumehesabiwa haki milele, bure,” sababu alikufa na akazikwa, na Mungu akamfufua tena asubuhi ya Pasaka. Kisha, Mungu alionyesha ya kwamba ilikuwa imekubalika, mambo yote aliyofanya. Kila kitu kiliisha kulipiwa, unaweza kuwa huru sasa! “Alipofufuka, akanihesabia haki bure milele.” Lo, hamna mtu anayeweza kujua, anayeweza kuwazia ile siku kuu Yeye alipofufuka; na Malaika waliiona, katika Mbingu za mbingu, hao Malaika waliimba sifa za Mungu, na wakafurahia huku wale watakatifu wa Agano la Kale walipofufuka Peponi. Haleluya! “Alipofufuka, akanihesabia haki.” Mbingu zikatetemeka, nchi ikatetemeka, peponi kukatetemeka, na kuzimu kukatetemeka. Aliposikia Sauti kubwa, Yeye akafufuka toka kaburini! “Alipofufuka, akanihesabia haki bure milele.” Lo, jamani!

⁴⁵ Basi watakatifu wanaokufa katika Yeye wanaweza kuuimba huu, tunapotazama neema ya ajabu huku, aliyotenda. Mnaona, Mungu alitia muhuri kibali Chake, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, bali ninyi mtaniona, kwa maana nitafufuka katika wafu nikae pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari; kama uthibitisho, na hakikisho ya kwamba yale aliyosema Mungu ni kweli, na yale nisemayo ni kweli,” Yesu akasema. “Nitakuja katika mfano wa Roho

Mtakatifu. Nitafanya maskani Yangu pamoja nanyi, na kuishi pamoja nanyi milele.” Basi watakatifu walio na tumaini hilo la ufufuo mioyoni mwao, wanaweza kuimba huu.

Bali katika—katika hiyo asubuhi yenye nuru
na isiyo na mawingu wakati hao waliokufa
katika Kristo watapofufuka,
Na kushiriki utukufu wa ufufuo Wake;
Wakati hao wateule Wake watakapokusanyika
makwao ng’ambo mbinguni, (wakiwa na
hakikisho kamilifu, wakiwa na Muhuri wa
Mungu, wakiwa na risiti iliyoandikwa na
Mungu Mwenyewe)

Majina yaitwapo kule ng’ambo nitakuweko.

Lo, akaja na akasema, kutoka kwa yeye aliyesema:

Maishani, alinipenda. Kifoni, akaniokoa.

Alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu.

Lo!

Alipofufuka, akanihesabia haki bure milele.

⁴⁶ Dhambi zimesamehewa. Dhabihu hizi zote zingelikuwa hadithi, dhabihu hizi zote zingalishindwa. Bali katika asubuhi ya Pasaka, alipofufuka, Mungu alithibitisha ya kwamba Yeye alikubali. Si ajabu, inaitea moyo wangu halleluya! Si ajabu inanifanya kusimama mauti yanaponikabili! Huwafanya watu waite yale mambo yasiyokuweko, kama kwamba yako! Mbona basi? “Alipofufuka, alinihesabia haki.” Unajuaje ya kwamba amefufuka? Kwa maana amefufuka mioyoni mwetu, akatuhesabia haki bure milele!

⁴⁷ Miaka arobaini baadaye, alipokuwa amesimama, akiwazungumzia watoto Wake, nguru za uvutano zikaaza kulegea. Kazi ilikuwa imemalizika. Deni ilikuwa amelipiwa. Alikuwa na risiti mkononi Mwake. Ilikuwa risiti ya Mungu. Alikuwa amepata watoto, Kanisa, waamini. Dhambi yote ilikuwa imeshindwa. Njia ilifanywa wazi. Yeye hangekaa duniani tena. Ni nini kinachotushikilia hapa? Nguvu za uvutano. Uvutano ukaanza kuvunjika, ukapoteza nguvu zake. Kwa nini? Ilikuwa imekwisha wakati huo. Kukatokea nini? Akaanza kuinuka kutoka ardhini.

⁴⁸ “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe,” ikasema midomo Yake. “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokolewa, asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Kwa Jina Langu watatoa pepo wachafu. Watanena kwa lugha mpya. Kama watashika nyoka ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru kamwe. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Kwa maana Mimi ni hai. . . Uvutano umeondoka Kwangu. Dhambi ilinishikilia, nilikufa kwa ajili yenu. Mungu amethibitisha hayo,

na akatoa risiti ya ufufuo. Na kwa maana Mimi ni hai, ninyi nanyi mwaishi pia! Siku moja nitarudi.”

⁴⁹ Siku moja yu aja, lo siku yenye utukufu! Kisha wakati... Kuishi, kufa, kuzikwa, kufufuka, kuja, tumaini la Kanisa leo!

Maishani, alinipenda. Kifoni, akaniokoa.
Alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu.
Alipozikwa, akanihesabia haki bure milele.
Yuaja siku moja, lo, siku tukufu!

Ni nini? Mambo matano katika herufi tano, J-e-s-u-s (Yesu).

Maishani, alinipenda. Kifoni akaniokoa.
Alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu.
Alipofufuka, akanihesabia haki bure milele.
Yuaja siku moja, lo, siku tukufu!

⁵⁰ Tunatazamia Kuja Kwake kwa Pili! “Na moja ya asubuhi hizi zenye nuru na zisizo na mawingu wakati hao waliokufa katika Kristo watakapofufuka, na kushiriki katika utukufu wa kufufuka huko; wakati wateule Wake watakapokusanyika makwao ng’ambo ya mbingu, majina yaitwapo kule ng’ambo, nitakuweko.” Kwa nini? Nina risiti. Yeye alifufuka! Wajuaje? Yuaishi moyoni mwangu. Yeye yuaishi mioyoni mwa watoto Wake.

⁵¹ Wazieni hayo, marafiki. Kidimbwi kitakuwa tayari katika muda mchache, maji yenye joto, kwa ajili ya ibada ya ubatizo, mara tutakaporudi.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mchache.

⁵² Nashangaa leo, iwapo mna mmoja miogoni mwetu, ama wengi ambao hawajathamini Dhabihu hii kutosha kuikubali, na ungetaka kukumbukwa katika maombi, kwamba Mungu atanena kiajabu moyoni mwako, upate kukubali Dhabihu Yake, kutakaswa kwa nafsi yako.

⁵³ Na kumbukeni ya kwamba leo tunasherehekea si wakati tu wa kuvalia kofia mpya na kuvalia nguo mpya; ambavyo ni sawa, ni mfano wa kitu kipya. Mungu alitenda jambo jipya. Ambalo, ni sawa. Si hayo tu. Pasaka haimaanishi hayo. Wapenzi, sungura wa Pasaka ama mayai ya Pasaka, na kuku wadogo weupe, na kadhalika, hilo silo wazo lake, ndugu.

⁵⁴ Pasaka ni ushindi, ni ushindi ambao Mungu alitoa juu ya dunia, ya kwamba Yeye alimfufua Mwanawe katika wafu. “Na ye yote amwaminiye, asipotee, bali awe na Uzima wa Milele.”

⁵⁵ Ufufuo unaweza kuwa maishani mwako. Iwapo hauna huo, je, waweza kumwinulia mkono wako asubuhi ya leo, huku mkiinamisha vichwa vyenu. Mkisema haya, “Mungu, nikumbuke, kusudi (huo) Uzima wa ufufuo uwe moyoni mwangu.” Mwaweza kuinua mikono yenu na kusema, “Niombee mimi, Ndugu Branham, ninapouinua mkono wangu?” Bwana akubariki. Bwana akubariki. Kuna mwingine atakayeinua

mkono wake, aseme, “Niombe, ndugu, mimi ninataka kuupokea huu Uzima wa ufufuo?”

Katika hiyo asubuhi yenye nuru na isiyu
na mawingu, (wazia hayo tunapoimba)...

Kristo watakapofufuka,
Na kushiriki utukufu wa ufufuo Wake;
Wakati hao wateule Wake watakapokusanyika
Makwao ng'ambo za mbingu,
Majina yaitwapo kule ng'ambo nitakuwako.

Majina yatakapoitwa huko ng'ambo,
Majina yatakapoitwa huko ng'ambo, (Sasa
iwapo huna hakika, hakikisha, sasa)...
yatakapoitwa huko ng'ambo,
Majina yatakapoitwa huko ng'ambo,
nitakuwako.

Na tumtumikie Bwana tangu...(jambo lile
lile)...jua,
Hebu na tuzungumze...

⁵⁶ Basi ninyi mlio Wakristo, mbona msimwekee Mungu nadhiri, mkamfanyie kazi na kumtumkia kwa bidii. Naam, mtu mwingine na amwinulie mkono.

Na majina yatakapoitwa huko ng'ambo
nitakuweko.
Majina yatakapoitwa huko ng'ambo,
Majina yatakapoitwa huko ng'ambo,
Majina yatakapoitwa huko ng'ambo,
nitakuweko.

⁵⁷ Mungu mpendwa, unaona kila moyo humu, na unajua nia na shabaha. Naomba kwa ajili ya rehema. Mungu, tujalie, ya kwamba rehema itaonyeshwa kwa watu hawa. Wamekuja asubuhi hii kwa ajili ya wakati huu wa kuabudu. Wamekuja ha—hapa kusikia Neno Lako, nasi tumelinena.

⁵⁸ Wewe ulipoishi, hapakuwepo maisha kama Yako. Kufani, ilikuwa Ndiwe tu ambaye angekufa namna hiyo. Ulipozikwa, uliondolea mbali dhambi zetu; ulipozichukua dhambi za watu, ulizipeleka kwenye Bahari ya Usahaulifu. Lakini, ulipofufuka, ulituhesabia haki bure milele. Nasi tumesimama leo tukiingoja Kuja Kwako.

⁵⁹ Mungu awabariki. Tusaidie. Tunatambua hatuna wakati mwingi zaidi, kwa sababu uko mlangoni. Na wo wote... Na saa moja tangu sasa, kulingana na wanasayansi, mataifa yangeangamizwa. Nasi tunaomba, Mungu, tunaposimama asubuhi hii ya Pasaka karibu sana na Kuja Kwake, tumaini la Kanisa. Maelfu wengi wamelala kule katika mavumbi ya ardhi, walingoja wakati huo, nafsi zao zikiwa chini ya madhabahu, zikilia, “Hata lini, Bwana? Hata lini?” Naomba, Mungu, ya kwamba utanena nasi. Na hebu tukumbuke ya

kwamba hata tufanye nini hapa duniani, ni kidogo sana. Na jambo pekee tunaloweza kufanya sasa, ni kungoja Kuja Kwako, na kumtangazia kila mtu. Ujumbe huu ni muhimu sana. Na tuutangazie watu, upesi, kwamba waweza kuja wakati wo wote. Kabla bomu hizi wanazonena habari zake, na makombora haya, yanaweza kumiminiwa maelfu yao walio duniani katika dakika moja; kabla hayo hayajatendeka, Wewe umeahidi kuja, Bwana, kuwachukua watu Wako. Itakuwa hivyo, Bwana. Kwa hivyo, dakika yo yote, kungekuwa na ufufuo, Pasaka ya Kanisa; ufufuo kutoka kwa maisha haya yenye dhambi, kuingia Uzima wa Milele, kupitia kwa Kristo. Sikia maombi yetu.

⁶⁰ Na leo, tunapoendelea kwenye ibada zingine, kuingilia mafundisho ya shule ya Jumapili, Ee, Bwana, nena nasi tena, na mioyo mingi na ihuishwe kiajabu. Na waje kwa dazan nyingi huku kidimbwini asubuhi hii, asubuhi hii ya Pasaka, kuzikwa pamoja na Bwana Yesu, wakikubali Dhambihu Yake. Haidhuru wao niwa kanisa gani, ama ni dhehebu gani wanaloshiriki nalo, hiyo haimaanishi kitu. Bali je, wao wamepokea ile Dhambihu? Je, wao wanakiri ya kwamba wao si wazuri, ya kwamba Yesu ndiye tu aliye mwema? Yeye alikufa kwa ajili yetu, badala yetu. Naye alichukua dhambi zetu akazizika, nasi tunasimama peke yetu ndani Yeye. Makanisa yetu hayawezi kuzika dhambi zetu, maisha yetu wenyewe hayawezi kuzika dhambi zetu, bali Kristo alizika dhambi zetu katika bahari ya Usahaulifu. Mungu, tujalie ya kwamba mambo haya yatakuwa ya utukufu mbele Zako.

⁶¹ Kisha usiku wa leo, Bwana, na uje katika uweza wa kufufuka Kwako, na utikise mahali hapa padogo kuliko vile pamewahi kutikiswa. Na ishara na maajabu yaonekane. Yarudie, kama ilivyokuwa Jumapili kadhaa zilizopita, Bwana, wakati wagonjwa na walioteseka waliponywa kiajabu. Tunaomba ya kwamba itakuwa hivyo tena usiku wa leo, kwa ajili ya utukufu Wako, Bwana.

⁶² Tusamehe makosa yetu sasa, Bwana, na hii iwe Pasaka halisi kwa wengine wetu, Pasaka halisi kwetu sote. Na wengine wa wale ambao hawajajua baraka za pasaka zilikuwa nini, na iwe ni leo ambapo Kristo atainuka mioyoni mwao, na tumaini lipya, na Maisha mapya. Waelekeze kalvari. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁶³ [Mahali patupu kwenye ukanda—Mh.] Wangapi wenu wanampenda Bwana, hebu inueni mikono yenu. Lo, jamani, hiyo ni ajabu!

⁶⁴ Nasikia una mtoto wa kuwekwa wakfu, Ndugu McDowell. Utarudi kwa ajili ya ibada ya shule ya Jumapili, unaweza? Sawa, hiyo itakuwa sawa. Mtu fulani ataweka watoto wakfu. Rudi wakati huo tafadhali, ikiwa hiyo ni sawa.

⁶⁵ Na sasa tutawaruhusu wasikizi waondoke kwa muda mchache, kusudi mpate kwenda makwenu mkale kiamsha

kinywa, kisha mkarudi tena. Tuna furaha ya kwamba mlikuwa humu.

⁶⁶ Basi na tusimame tu. Wimbo ule ule tuliouimba muda mchache uliopota, “Katika hiyo asuhubi yenye nuru na isiyo na mawingu. . .” Wangapi walio na matumaini kwayo, na tuone mikono yenu. Amina.

Katika hiyo asubuhi yenye nuru na isiyo na
mawingu wakati waliokufa katika Kristo
watakapofufuka,

Na kushiriki utukufu wa ufufuo Wake;
Wakati waliookolewa duniani
watakapokusanyika kule ng'ambo ya . . .



KUISHI, KUFA, KUZIKWA, KUFUFUKA, KUJA SWA59-0329s

(Living, Dying, Buried, Rising, Coming)

MFULULIZO WA UJUMBE WA PASAKA

Ujumbe huu wa Ndugu William Marriion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kwenye ibada ya Mapambazuko ya Jumapili ya Pasaka mnamo mwezi wa Marchi 29, 1959, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org